KAFITI FOUNDATION

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

## Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza

Kafiti Foundation ni shirika lisilo la kiserikali linalojikita katika kuziondoa jamii kwenye umaskini kwa kuleta maendeleo ya jamii kwa njia endelevu kupitia miradi ya uwezeshaji wa kiuchumi, elimu, afya, ulinzi wa mazingira, na biashara ndogo ndogo.

Tunakaribisha waombaji wenye ujuzi, ari, na dhamira ya kuleta mabadiliko kujiunga na timu yetu. Kafiti Foundation ni mwajiri wa fursa sawa. Waombaji wote wanakaribishwa bila kujali jinsia, dini, kabila au ulemavu.

## A: NAFASI ZA MDA MREFU

| Nafasi | Majukumu Muhimu |
|---|---|
| Meneja wa Miradi | Kusimamia miradi, timu na bajeti |
| Msaidizi wa Utawala | Usaidizi wa shughuli za kila siku za ofisi |
| Dereva (Nafasi 2) | Usafirishaji wa wafanyakazi na mali za ofisi |
| Muhudumu wa Usafi | Kusafisha na kudumisha usafi wa ofisi |
| Afisa Mawasiliano / PR | Uhusiano na jamii, vyombo vya habari na wadau |
| Katibu / Huduma kwa Wateja | Kupokea wageni na usimamizi wa mawasiliano ya ofisi |

| Nafasi | Majukumu Muhimu |
|---|---|
| Afisa Ufuatiliaji & Tathmini (M&E) | Kufuatilia maendeleo ya miradi na ripoti |
| Mpishi | Kupika na kuhakikisha chakula kwa wafanyakazi na wageni |
| Graphic Designer | Kubuni graphics, mabango, poster na vifaa vya mitandao |
| Photo Shoot / Photographer | Kupiga picha na kurekodi matukio ya miradi na shughuli |
| Afisa Usafirishaji / Bodaboda | Kusafirisha nyaraka, vifaa na wafanyakazi ndani ya Mwanza |
| Mlinzi | Muombaji awe na mafunzo rasmi ya ulinzi na kipaumbele cha pekee kitatolewa kwa mkazi wa Kata ya Kahama. |

- **Tarehe ya Kutangazwa:** 26Januari 2026.
- **Muda wa Mwisho:** 06 Februari 2026.
- **Mrejesho wa maombi :** waombaji watakaokidhi vigezo na kuchaguliwa watajilishwa kwaajili ya usaili. Andika nafasi unayoomba kwenye kichwa cha barua pepe/bahasha.
- **Mahali pa kazi:** Makao makuu (HQ) Kafiti Foundation, Barabara ya Magaka, Kahama, Ilemela, Mwanza.
- **Sifa za Waombaji:** Uzoefu na ujuzi utazingatiwa .

KAFITI FOUNDATION

- **Kipaumbele:** Kipaumbele cha kipekee kitatolewa kwa waombaji ambao ni wakazi wa Wilaya ya Ilemela, Mwanza.

- **Uadilifu:** Ari ya kufanya kazi kwa bidii, uaminifu, na nidhamu ya hali ya juu.

- **Leseni:** Kwa nafasi za Dereva na Bodaboda, ni lazima kuwa na leseni halali ya udereva kulingana na daraja la chombo husika.

- **Uwasilishaji:** Barua na CV zitumwe kwenye barua pepe: info@kafitifoundation.org Au wasilisha moja kwa moja makao makuu ya Kafiti Foundation yaliyopo Barabara ya Magaka, Kahama, Ilemela, Mwanza

- **Tahadhari:** Hakuna malipo yoyote yanayohitajika katika hatua yoyote ya mchakato wa ajira.

KAFITI FOUNDATION

# B: NAFASI 50 ZA MDA MFUPI

## Nafasi Zinazotangazwa:

Wakusanyaji wa Takwimu — Nafasi 46.
Wahudumu wa Kuingiza Takwimu — Nafasi 4.
**Eneo la Utekelezaji wa Kazi:** Kata zote 19 na mitaa yote 171 ya Wilaya ya Ilemela.

## 1. Majukumu ya Kazi:

- Kupata ridhaa ya washiriki (informed consent) na kuwaeleza madhumuni ya mradi.
- Kukusanya takwimu kwa kutumia dodoso rasmi za mradi.
- Kuhakikisha taarifa zote zimejazwa kikamilifu, kwa usahihi na kwa uwazi.
- Kuhakiki taarifa zinazoonekana za biashara (aina ya biashara, eneo na hali ya uendeshaji).
- Kuwasilisha dodoso zilizojazwa kila siku kwa msimamizi wa eneo.
- Kuripoti changamoto, mapungufu au dosari zozote za taarifa kwa wakati.
- Kuzingatia maadili ya utafiti, usiri wa taarifa na ulinzi wa takwimu.
- Kushiriki kikamilifu katika mafunzo ya maelekezo na tathmini ya kazi.

KAFITI FOUNDATION

## Sifa za Mwombaji:

- **Elimu:** Kidato cha Nne (Form IV), Cheti au Stashahada.
- Awe mkazi wa Wilaya ya Ilemela na mwenye uelewa mzuri wa kata au mtaa husika.
- Awe na uwezo mzuri wa mawasiliano, umakini kazini na nidhamu ya kazi.
- Awe tayari kusafiri na kufanya kazi katika mitaa atakayopangiwa kwa muda wote wa mradi.
- Waombaji wenye uelewa wa matumizi ya Google Forms na wenye simu janja watapewa kipaumbele.

## Jinsi ya Kuomba:

### Nyaraka Zinazohitajika

- Wasifu (CV) wenye mawasiliano ya mwombaji.
- Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- Barua fupi ya maombi.
- Barua ya utambukisho kutoka mwenyekiti wa serikali ya mtaa.

## Mwisho wa kuwasilisha maombi:

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 06 February 2026 kwa kufika Makao Makuu ya Kafiti Foundation, Mtaa wa barabara ya Magaka, Kahama, Ilemela, Mwanza, au kutuma kwa barua pepe: info@kafitifoundation.org Simu: +255 788 348 873